

ilikuwa ni kero kubwa kutokana na moshi mzito. Pia hatua ya kusitisha ililenga kutoa nafasi ya kufanya thathmini ya athari za shughuli za uzalishaji nondo kwa watu na mazingira na ukarabati ili kuweka mfumo mzuri wa kutolea moshi na majitaka kiwandani hapo.

Hata hivyo, kutokana na juhudi za Baraza na wadau wake, tulitegemea kupata ushirikiano wa dhati toka uongozi wa kampuni hiyo katika kushughulikia tatizo hilo kama ilivyoelekezwa na wataaalamu kwa nyakati mbalimbali. Malalamiko ya wananchi yalikuwa mengi na athari kwa afya za watu zilikuwa dhahiri. Kutokana na sheria kuwepo rasmi na kuanza kutumika, kampuni hii imezuiliwa kuendesha shughuli za uzalishaji (Prohibitory Notice) mpaka hapo marekebisho matatizo makuu yaliyobainishwa yatakapokamilika na kukaguliwa kuwa yanaridhisha. Ikumbukwe kuwa mazingira ni maswala mtambuka hivyo ushirikishwaji wadau ni muhimu, hivyo Baraza limeshirikiana na wadau wengine kufikia uamuzi huu wa kutoa notisi ya kusitisha uzalishaji wa kiwanda kama Sheria ya Mazingira (2004) inavyoelekeza. Wadau wengine hao ni; Manispaa za Kinondoni na Ilala, Jiji, Mkaguzi wa Viwanda, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TIRDO, Idara ya mazingira (DOE), BRELA na Jeshi la Polisi. Kwa mantiki hiyo, wawekezaji wengine wanashauriwa kuepukana na usumbufu wa aina hii kwa kufuata sheria na kutoa ushirikiano kwa Baraza na wadau wengine katika kutunza mazingira.



MKURUGENZI MKUU
BARAZA LA TAIFA LA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA
MAZINGIRA